

Mkataba huufanyika leo 25 mwezi 01 mwaka, 2022

KATI YA

MICHAEL NDEONASIA MACHA wa , Dar es Salaam, ambaye katika Mkataba huu atajulikana kwa upande mmoja kama "MWENYE NYUMBA."

NA

ATLANTA GLOBAL LIMITED, S.L.P 32521 wa Dar es Salaam ambaye kwa upande mwingine ataitwa "MPANGAJI"

KWA HIVYO, Mwenye Nyumba amekubali kwa hiyari yake mwenyewe kumkodisha nyumba iliyopo kwenye kiwanja na. 70, Block B, eneo la Mikocheni, wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam.

MASHARTI

1. Mkataba huu ni wa Mwaka kuanzia tarehe 01/01/2022 hadi tarehe 31/12/2022.
2. Kiwango cha Kodi ya pango itakuwa Shilingi Laki Moja (Tsh. 100,000/=) kwa mwezi.
3. Malipo ya kodi yatafanywa kwa kulipa kodi ya MWAKA yaani shilingi Milioni Moja na Laki Mbili Tu (Tsh.1 200, 000/=) ambayo italipwa mara moja wakati wa kusaini mkataba huu.
4. Mpangaji atatakiwa kulipa bili ya maji na usafi kwa kila mwezi na kuhakikisha eneo alilopangisha linakuwa katika hali ya usafi katika kipindi chote atakachokuwa amepanga katika eneo husika.
5. Mkataba huu utasitishwa mara moja iwapo mpangaji atashindwa kulipa kodi ya pango.
6. Mpangaji atatakiwa kueleza nia yake ya kusaini Mkataba mpya mwezi mmoja kabla ya Mkataba huu kuisha.
7. Mkataba huu utatekelezwa kwa Misingi ya kuheshimiana na kuelewana kwa kuzingatia haki za kila mhusika wa Mkataba huu.

8. Kwamba endapo Mpangaji ataendelea baada ya kodi yake kuisha atatakiwa ajaze mkataba mpya ambao unaweza kuwa na masharti mapya hususani kwa kiwango cha kodi.
9. Mpangaji atatumia nyumba hiyo kwa matumizi ya biashara aliyoisema tu, endapo atatumia nyumba hiyo kwa matumizi mengine itabidi yafanyike maelewano na mwenye nyumba.
10. Wahusika wanakubaliana kwamba upande wowote unaweza kuvunja mkataba kwa kuupa upande mwingine notisi ya siku thelathini (30).
11. Iwapo itatokea kutoelewana baina ya mpangaji na mwenye nyumba kuhusiana na mkataba huu, tofauti zao watazimaliza kwa kutumia wasuluhishi na ikishindikana hapo suala zima litapelekwa kwenye vyombo vya sharia.

Mkataba huu umeshuhudiwa na kusainiwa na;

MWENYE NYUMBA: MICHAEL NDEONASIA MACHA; Sahihi: 

MPANGAJI: OMARI SAID MUHALI
KWANIABA YA : ATLANTA GLOBAL LIMITED Sahihi: 

MBELE YA:

Jina: ALFRED OCTAVIAN LYARUU

Saini: 

Anwani/Simu: S. L. P 19927/ 0714547998



WADHIFA: WAKILI

WHT - 120,000/=

SD - 12,000/=

TZS 132,000/=

f

26-01-2022